Jarida la

Ligi Kuu

Juni 2026

Msimu Umetamatika





Ligi Kuu ya NBC,
Ligi ya Championship ya NBC na First League

www.ligikuu.co.tz

Yaliyomo

Kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu.....1

Mabingwa wa Kihistoria..... 4

Mfalme wa Hat-Trick 5

Filimbi ya Mwisho Ligi Kuu ya NBC 12

Mitindo na Ubunifu..... 19

Ligi ya Championship..... 22

First League..... 29

Ijue Kanuni..... 32







MAELEZO YA UCHAPAJI

Jarida hili huchapishwa kila mwezi na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania - TPLB

Mhariri Mkuu
Cornel Barnabas

Mhariri Habari
Yahaya Abushehe

Mhariri Msaidizi
Honest Mwanitega

Mpiga Picha
Loveness Bernard

Msanifu Kurasa
James Onesmo

Wachangiaji
Salma Seif
Pancras Remidius
Cynthia Michael
Sakina Abdoul
Collins Mwesigwa



Bodi ya Ligi Tuu Tanzania

Ghorofa na 14, NSSF Mafao House,
Barabara ya Uhuru - Ilala,
Dar es Salaam
S. L. P 79041 Dar es Salaam

www.ligikuu.co.tz
info@ligikuu.co.tz

Ligi Kuu

ligikuu | championshiptz | firstleague

tplboard

ligikuu

Ligikuu

LIGI KUU TV

Msimu wa Ligi 2025/2026 Umetamatika

Mwezi Juni umekuwa wa kipekee kwa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, kwani ni mwezi ulioshuhudia tamati ya Ligi zetu na kuhitimisha msimu wa soka kwa ngazi mbalimbali za ligi zinazosimamiwa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania.

Kwa niaba ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Rhino Rangers kwa kutwaa ubingwa wa First League, Geita Gold kwa kuwa mabingwa wa NBC Championship, na Young Africans kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC. Mafanikio haya yanaonyesha ushindani mkubwa, uwekezaji wa klabu, na juhudi za wadau wote wa soka nchini.

Msimu huu umeonyesha maendeleo makubwa katika uendeshaji wa ligi zetu. Tumeendelea kuboresha usimamizi wa ratiba, kuimarisha viwango vya waamuzi, kuendeleza matumizi ya teknolojia katika shughuli za ligi, na kuongeza ushiriki wa wadhamini pamoja na mashabiki. Hatua hizi zimechangia kufanya ligi zetu kuwa na mvuto zaidi ndani na nje ya Tanzania.

Tunatambua mchango wa klabu, waamuzi, wadhamini, vyombo vya habari, mashabiki na wadau wote wa soka ambao wameendelea kushirikiana nasi katika kuhakikisha mashindano yanaendeshwa kwa ufanisi. Ushirikiano huu ndio msingi wa mafanikio tunayoshuhudia leo.

Tunapoifunga rasmi kalenda ya mashindano ya msimu huu, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania itaendelea kujitathmini na kuweka mikakati ya kuboresha zaidi mazingira ya ushindani, maendeleo ya klabu, na uzoefu wa mashabiki katika misimu ijayo.

Cornel Barnabas

Afisa Mtendaji Mkuu
Bodi ya Ligi Kuu Tanzania





YOUNG AFRICANS WAANDIKA HISTORIA LIGI KUU YA NBC.

Msimu wa 2025/26 wa Ligi Kuu ya NBC umefungwa kwa sura ya kipekee baada ya Young Africans kutwaa ubingwa na kuweka rekodi mpya ya kubeba kombe hilo kwa misimu mitano mfululizo.

Mafanikio hayo yanaendelea kuifanya klabu hiyo kuandika historia kama moja ya timu zilizotawala soka la Tanzania katika miaka ya karibuni kupitia matokeo mazuri, ubora wa kikosi na mwendelezo wa ushindani.

Young Africans walimaliza msimu wakiwa kileleni mwa msimamo wa ligi kwa alama 75 baada ya kucheza micheao 30, wakishinda 23, kutoka sare sita na kupoteza mchezo mmoja pekee.

Mbali na kukusanya alama nyingi zaidi mabingwa hao walitengeneza rekodi ya kuvutia katika takwimu za ushambuliaji na ulinzi. Walifunga jumla ya mabao 71, idadi iliyoonyesha ubora wa safu yao ya ushambuliaji, huku wakiruhusu mabao tisa pekee katika mechi zote 30 za ligi.

Safari ya mabingwa hao ilihitimishwa kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya JKT Tanzania katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo. Prince Dube aliifungia Young Africans bao la kwanza kabla ya Maxi Nzengeli kuongeza la pili, huku Laurindo Dilson akifunga bao la tatu na kuhitimisha msimu kwa ushindi uliowapa fursa ya kusherehekea ubingwa mbele ya mashabiki wao waliokuwa wamejitokeza.

Baada ya filimbi ya mwisho, hafla rasmi ya kukabidhi kombe la Ligi Kuu ya NBC ilifanyika uwanjani ikihudhuriwa na viongozi wa soka, wadhamini wa ligi, wadau mbalimbali wa mchezo pamoja na maelfu ya mashabiki waliojitokeza kushuhudia mabingwa wakitawazwa.

Sherehe hizo zilikuwa hitimisho la msimu mwingine wenye ushindani mkubwa na mafanikio makubwa kwa Young Africans.

Ubingwa wa msimu wa 2025/26 unakuwa wa tano mfululizo kwa Young Africans rekodi inayodhihirisha mwendelezo wa mafanikio yao katika soka la Tanzania ambapo katika kipindi hicho, klabu imeendelea kujenga utamaduni wa ushindi, ikitawala ligi kupitia kikosi chenye ushindani, benchi la ufundi lenye mbinu na uwezo wa kudumisha kiwango bora kila msimu.

Kumalizika kwa msimu wa 2025/26 kunafunga rasmi pazia la Ligi Kuu ya NBC baada ya miezi kadhaa ya ushindani mkali ulioshuhudia mapambano ya ubingwa, nafasi za kushiriki michuano ya kimataifa zilizochukuliwa na timu za Young Africans na Simba zilizopata uwakilishi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, pamoja na timu za Azam na Singida Black Stars zilizopata uwakilishi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Sasa macho ya wadau wa soka yanaelekezwa kwenye msimu wa 2026/27, ambapo Young Africans wataingia wakiwa mabingwa watetezi na timu nyingine zikiwa na dhamira ya kuvunja utawala huo. Swali kubwa litakalotawala msimu ujao ni kama kuna klabu itakayoweza kusimamisha safari ya ‘Wananchi’ au kama Young Africans wataendelea kuandika ukurasa mwingine wa historia ya soka la Tanzania kwa ubingwa wa sita mfululizo

- **Mechi: 30**
- **Ushindi: 23**
- **Sare: 6**
- **Kupoteza: 1**
- **Mabao ya Kufunga: 71**
- **Mabao ya Kufungwa: 9**
- **Tofauti ya Mabao: +62**
- **Alama: 75**

HUYU HAPA MFALME WA HAT-TRICK LIGI KUU YA NBC



Mshambuliaji wa Singida Black Stars raia wa Burundi, Mossi Ndumumwe, ameendelea kuthibitisha ubora wake mbele ya lango baada ya kuweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao matatu kwenye mchezo mmoja yaani (hat-trick) katika msimu wa 2025/26 wa Ligi Kuu ya NBC, mafanikio aliyopata katika ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Dodoma Jiji.

Hat-trick hiyo haikuwa pekee msimu huu bali imekuwa sehemu ya rekodi binafsi ya Ndumumwe dhidi ya wapinzani wake na hadi msimu unatamatika mshambuliaji huyo alifunga hat-trick mbili katika Ligi Kuu ya NBC moja dhidi ya Dodoma Jiji na nyingine dhidi ya Fountain Gate kwenye mchezo wa mzunguko wa 30.

Ndumumwe aliyesajiliwa dirisha dogo aliongeza nguvu kubwa katika safu ya ushambuliaji ya Singida Black Stars tangu alipojiunga na klabu hiyo huku kasi, utulivu akiwa ndani ya eneo la hatari na uwezo wa kumalizia nafasi vikimfanya kuwa mmoja wa washambuliaji wanaotegemewa zaidi kwenye kikosi cha Singida.

“Namshukuru Mungu na wachezaji wenzangu, peke yangu nisingeweza maana nimeingia dirisha dogo na nikapewa nafasi ya kuonyesha kipaji changu haikuwa rahisi ulikuwa ni msimu mgumu sana”alisema Ndumumwe

Rekodi yake ya hat-trick mbili inaweka jina lake kwenye kundi la washambuliaji wenye uwezo wa kubadili matokeo ya mechi peke yao kwani mabao hayo yamechangia kuwa mfungaji bora wa msimu wa 2025/2026 akiwa na mabao 17.



MATHEW TEGISI

Raia wa Kenya anaekipiga Pamba Jiji ndio mchezaji aliyefunga hat-trick ya pili ndani ya msimu wa 2025/2026 wakati wa mchezo wa mzunguko wa 27 wa Ligi Kuu ya NBC dhidi ya timu ya Mtibwa Sugar kwenye mchezo uliochezwa katika uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.



FABRICE WA NGOY

Fabrice Ngoy ni ‘Staa’ wa Namungo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo aliyekuwa mmoja wa wachezaji waliofunga hat-trick msimu huu, akifanya hivyo dhidi ya KMC, mabao yaliyochangia timu ya Namungo kusalia kwenye Ligi Kuu ya NBC na kumfanya aendelee kuwa mmoja wa wafungaji tegemeo wa timu hiyo.



ALLAN OKELLO

Ni raia wa Uganda anayekipiga kwenye timu ya Young Africans aliyejiunga na timu hiyo kwenye dirisha dogo la usajili, hakuwa nyuma kuonyesha ‘makeke’ yake na amefanikiwa kufunga hat-trick wakati wa mchezo kati ya timu yake na TRA United ikiwa ni ndani ya mzunguko wa 29 wa Ligi Kuu ya NBC hivyo kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji waliofunga mabao mengi ndani ya msimu huo.




5H-FSA
flySunBird


5H- FSA

FILIMBI YA MWISHO LIGI KUU YA NBC 2025/2026

Juni 30, 2026 haikuwa siku ya kawaida ya mpira wa miguu bali siku ambayo ndoto zilihitimishwa, historia ikaandikwa, na pazia la msimu mwingine wa kusisimua wa Ligi Kuu ya NBC likashushwa rasmi.



Kuanzia Dar es Salaam, Mbeya, Singida ,Tanga, Arusha na Lindi macho ya maelfu ya mashabiki yalikuwa viwanjani huku mamilioni wengine wakifuatilia kupitia televisheni, redio na kwenye mitandao ya kijamii michezo yote nane iliyoanza kwa wakati mmoja.

Hakukuwa tena na nafasi ya kurekebisha makosa, hakukuwa na raundi nyingine, kilichobaki kilikuwa ni dakika tisini za mwisho za safari iliyodumu kwa miezi kadhaa na filimbi zilipopulizwa kwa mara ya kwanza kila uwanja uliandika simulizi yake.

Young Africans waliokuwa na nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa ambao hadi siku ya mwisho ulikuwa haujapata mwenyewe walitoa hitimisho linalostahili kwa mashabiki wao, wakishinda 3-0 ugenini dhidi ya JKT Tanzania, Wakicheza kwa kujiamini, nidhamu na utulivu, wakipata ushindi uliosisitiza kwa nini walikuwa timu bora zaidi iliyostahili ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2025/26.

Kwa upande mwingine timu ya Simba iliyokuwa ikiifukuza Young Africans ilihitimisha msimu kwa ushindi wa 1-0 dhidi ya KMC iliyoshuka daraja ingawa ndoto ya kutwaa ubingwa kwa Simba haikutimia lakini walionyesha ushindani ulioufanya msimu wa 2025/26 kuwa wa kuvutia kutoka mwanzo hadi mwisho na hivyo Simba kuungana na Young Africans kwenye uwakilishi wa nchi katika Ligi ya Mabingwa Afrika msimu wa 2026/27.

'Matajiri wa Chamazi' timu ya Azam nao walimaliza kampeni yao kwa ushindi wa 2-0 dhidi ya Dodoma jiji na hivyo kumaliza kwenye nafasi ya tatu inayoipa nafasi timu hiyo kuiwakilisha Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Kama kulikuwa na uwanja uliowapa mashabiki burudani ya kipekee katika siku hii ya mwisho basi ulikuwa uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha ulioshuhudia mabao saba yakifungwa na kuifanya mechi hiyo kuwa moja ya michezo ya kusisimua zaidi ya msimu mzima baada ya Fountain Gate kuifunga Singida Black Stars mabao 4-3 ambayo licha ya kupoteza mchezo huo bado inaungana na Azam kama mwakilishi wa Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Uwanja wa Sokoine pekee ulitoa sare kwenye michezo ya mwisho ambapo Mbeya City ililazimishwa suluhu na TRA, Namungo ikiifunga 2-1 Mtibwa na kuishusha daraja rasmi kwenye uwanja wa Majaliwa, Lindi, Coastal Union ikiifunga Pamba Jiji 2-1 Mkwakwani, Tanga na kwenye uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma timu ya Prisons iliungana na Young Africans na kuwa timu pekee zilizoshinda ugenini siku hiyo baada ya kuifunga Mashujaa 1-0.

Siku ya mwisho ya Ligi Kuu ya NBC ilikuwa ya aina yake kwani Kombe lilikuwa kwenye helikopta iliyozunguka katika anga la uwanja wa Mej Isamuhyo na KMC, Dar es Salaam ambapo lazima bingwa angepatikana kwenye uwanja mmojawapo kati ya hivyo na angekuwa timu ya Simba au Young Africans na mwisho ilitua Isamuhyo na kukabidhiwa kwa Young Africans aliyeibuka Bingwa baada ya kukusanya jumla ya alama 75.

Baada ya juni 30, klabu zitaanza kupanga vikosi upya, usajili utaanza kuteka vichwa vya habari na makocha wataanza kupanga mikakati mipya huku wachezaji wakianza maandalizi ya kurudi wakiwa bora zaidi na mashabiki nao wataanza kuhesabu siku zilizobaki kabla ya filimbi ya kwanza ya msimu mpya wa 2026/27 kupulizwa tena Agosti 14, 2026.









Vinara wa namba Ligi Kuu ya NBC

Mbio za kuwania tuzo ya mfungaji bora wa Ligi Kuu ya NBC zimetamatika rasmi baada mzunguko wa 30 wa Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2025/2026 na ‘staa’ wa Singida Black Stars raia wa Burundi Ndumumwe Mossi akiibuka mfungaji bora baada ya kutupia mabao 17.

Ndani ya mabao hayo ya Mossi alifanikiwa kufunga mabao matatu kwenye mchezo mmoja yaani (hat-trick) mara mbili alizofunga dhidi ya Dodoma Jiji na Fountain Gate licha ya kusajiliwa dirisha dogo na ameiwezesha timu yake kufuzu kombe la Shirikisho Afrika.

Feisal Salum wa Azam anashika nafasi ya pili akiwa amefanikiwa kufunga mabao 15 licha ya kucheza nafasi ya kiungo, Feisal ameendelea kuthibitisha uwezo wake wa kufunga na kuisaidia timu yake katika nyakati muhimu.

Allan Okello wa Young Africans anashika nafasi ya tatu akiwa na mabao 14. Okello amekuwa mmoja wa wachezaji wenye ushawishi mkubwa msimu huu kutokana na ubunifu wake na uwezo wa kumalizia nafasi.

Mathew Tegisi wa Pamba Jiji ana mabao 11 idadi inayomfanya awe miongoni mwa washambuliaji waliokuwa na msimu mzuri. Akiwa sambamba na Fabrice Ngoy, ambaye pia amefikisha mabao 11 na kuendelea kuwa tishio kwa safu za ulinzi za wapinzani.

Fabrice Ngoy ni mshambuliaji anaekipiga Namungo ambaye ndani ya msimu wa 2025/2026 amefanikiwa kutikisa nyavu mara 11 ikiwemo kufunga hat-trick moja dhidi ya KMC.

Ukiachana na ‘wakali’ wa kufunga mabao, msimu wa 2025/2026 wa Ligi Kuu ya NBC wapo wachezaji waliohusika kwenye pasi za mabao katika michezo mbalimbali ya ligi hiyo, Hawa hapa vinara:

Ellie Mpanzu
Ni kiungo wa timu ya Simba ambaye licha ya kutokuanza msimu vizuri lakini ameweza kuibuka kinara wa pasi za mwisho baada ya kutoa pasi 10 za mabao.

“Haikuwa ligi rahisi tumepambana kama timu kuhakikisha tunafanikisha malengo, sikuanza vizuri msimu lakini Mungu amenisaidia nimemaliza msimu nikiongoza kwa kuwa na pasi za mabao nyingi” amesema Mpanzu.

Feisal Salum
Kiungo wa timu ya Azam ambaye hayupo mbali na Mpanzu akiwa na pasi za mwisho tisa ndani ya msimu huu ambapo hata hivyo kiungo huyo ameshindwa kuivunja rekodi yake mwenyewe aliyoweka msimu uliopita wa Ligi Kuu ya NBC ya kupiga pasi za mwisho 13.

Allan Okello
Ni kiungo wa timu ya Young Africans aliyesajiliwa dirisha dogo akitokea timu ya Vipers ya Uganda ambaye licha ya ugeni ndani ya Ligi ameweza kuweka pasi za mwisho nane na kuisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC msimu huu .

Zabona Mayombya
Ni mchezaji anaekipiga katika timu ya Pamba Jiji ya Mwanza ambaye katika msimu wa 2025/2026 wa Ligi Kuu ya NBC ameweza kuweka pasi za mabao nane akivunja rekodi yake ya msimu uliopita ambapo alikuwa na pasi tano pekee .

Clatous Chama
Kiungo wa timu ya Simba amefanikiwa kuweka pasi za mwisho saba ndani ya msimu wa 2025/2026 wa Ligi Kuu ya NBC wakati msimu uliopita alikuwa na pasi tatu pekee.

Prince Dube
Mshambuliaji wa timu ya Young Africans raia wa Zimbabwe ambaye msimu huu ameweza kuweka pasi saba za mwisho huku akiwa na mchango mkubwa wa kuiwezesha timu ya Young Africans kutwaa ubingwa.

Maxi Nzengeli
Kiungo wa timu ya Young Africans akiwa na pasi saba sawa na mwenzake Dube, hata hivyo ameshindwa kuifikia rekodi yake ya msimu uliopita ya pasi za mwisho 10 huku uwepo wao ukionyesha ushindani mkubwa katika Ligi Kuu ya NBC.



Kuu ya NBC ulikuwa na ushindani mkubwa kwa upande wa magolikipa ambapo kila mmoja alijitahidi kuhakikisha timu yake inapata alama ili kuweza kusonga mbele.

Djigui Diarra
Minda mlango wa timu ya Young Africans ambaye ndiye Kinara wa hati safi akiwa ameiwezesha timu yake kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC huku akikusanya hati safi 18.

Mahamodou Kassali
Ni usajili wa dirisha dogo ambao ulifanywa na timu ya Simba baada ya mlinda mlango wao Moussa Pinpin Camara kuumia jeraha la muda mrefu, hata hivyo Pamoja na ugeni kwenye Ligi Kassali amefanikiwa kukusanya hati safi 16 na kushika nafasi ya pili nyuma ya Diarra .

Aishi Manula
Ni golikipa anaekipiga timu ya Azam akiwa ameiwezesha timu yake kuvuna hati safi 14 pamoja na kushika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC na pia timu yake kufuzu kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika.

Jean Noel
Golikipa wa timu ya TRA United, amefanikiwa kupeperusha vyema bendera ya timu hiyo kwa kukusanya hati safi 13 ndani ya msimu wa 2025/2026 wa Ligi Kuu ya NBC.

Zuberi Foba
Golikipa wa namba mbili wa timu ya Azam amefanikiwa kukusanya hati safi tisa hivyo kuifanya timu yake kuwa miongoni mwa timu zilizokusanya hati safi nyingi zaidi ndani ya msimu wa 2025/2026 ikiwa imekusanya 24.



Kazi na Dakika 2,700 za ‘Jasho na Damu’

Si rahisi kwa mchezaji kudumu uwanjani kwa msimu mzima katika soka la kisasa bila kukosa hata dakika moja. Majeraha, adhabu za kadi, mabadiliko ya kiufundi au kupumzishwa ni mambo yanayowakumba wachezaji wengi. Hata hivyo, kwa Hussein Bakari Kazi, hayo yote hayakuwa kikwazo, beki huyo wa timu ya Namungo ameweka rekodi ya kipekee msimu wa 2025/26 kwa kuwa mchezaji pekee aliyecheza michezo yote 30 ikiwa na jumla ya dakika 2,700.

Rekodi hiyo si ya kawaida hata kidogo. Ni ushahidi tosha wa utimamu wa mwili, nidhamu na kiwango cha kuaminika alichokijenga mbele ya benchi la ufundi la timu yake ambapo kwa msimu mzima alikuwa nguzo muhimu ya ulinzi akiwasaidia ‘wauaji wa kusini’ kuepuka kushuka daraja na kusalia kwenye Ligi Kuu ya NBC msimu ujao

Kila mchezo ulipoanza jina lake lilikuwa sehemu ya kikosi cha kwanza na kila filimbi ya mwisho ilipopulizwa bado alikuwa amesimama uwanjani, huo ni uthibitisho wa mchezaji ambaye si tu ana uwezo wa kucheza soka vizuri, bali pia anaweza kubeba majukumu makubwa kwa msimu mzima bila kupoteza kiwango chake.

Safari ya Hussein Bakari Kazi katika Ligi Kuu ya NBC haikuanza leo kwani kabla ya kuwa nguzo muhimu ya Namungo aliwahi pia kuvaa jezi za timu kama Simba na Geita Gold alipopata uzoefu mkubwa wa kucheza katika mazingira yenye ushindani wa hali ya juu, uzoefu ambao umeonekana wazi msimu huu kupitia uimara wake, utulivu wake na uwezo wa kuhimili ‘presha’ katika kila pambano.

Kwa mchezaji anayekipiga nafasi ya ulinzi, dakika 2,700 zina maana kubwa zaidi kuliko takwimu. Zinamaanisha kukabiliana na washambuliaji hatari wa ligi kwa msimu mzima, kufanya maamuzi sahihi kila mchezo na kuendelea kuwa chaguo la kwanza, hii ni rekodi inayodhihirisha kwamba mafanikio ya timu hayajengwi na wafungaji pekee, bali pia na walinzi wanaohakikisha usalama wa goli kila wanapokuwa uwanjani.

Katika msimu ambao uliwashuhudia nyota wengi wakivunja na kuweka rekodi mbalimbali, Hussein Bakari Kazi amejiweka katika kundi la wachezaji waliothibitisha kuwa kujituma uwanjani ni silaha muhimu katika soka la ushindani. Dakika zake 2,700 alizocheza zitabaki kuwa alama ya msimu wa 2025/26 na mfano kwa kizazi kipya cha wachezaji wanaotamani kufika juu zaidi.



JUMA ISSA ABUSHIRI: KINDA WA MWEZI JUNI.

KATIKA kila msimu wa soka kuna wachezaji wachache ambao hawahitaji muda mrefu kuwashawishi mashabiki kuhusu uwezo wao wanapokuwa ndani ya uwanja hivyo wanaingia uwanjani, wanacheza kwa kujiamini, wanaonyesha ubora wao na kuacha kila mtu akizungumza kuwahusu. Mmoja wa vijana hao ni Juma Issa Abushiri.

Akiwa miongoni mwa vipaji vinavyoendelea kukua ndani ya timu ya Fountain Gate, Abushiri ameonyesha kuwa umri si kigezo cha kucheza soka la ushindani, utulivu wake akiwa na mpira, uwezo wa kusoma mchezo, pamoja na nidhamu ya kutekeleza majukumu yake uwanjani vimemfanya kuwa mmoja wa vijana waliovutia zaidi katika kipindi cha mwezi Juni.

Katika mechi za mwisho za msimu Abushiri aliendelea kupewa nafasi na benchi la ufundi, jambo lililoonyesha imani kubwa waliyonayo kwa maendeleo yake ambapo kila alipopata nafasi alionyesha ari ya kupambana, matumizi mazuri ya mpira na uwezo wa kushirikiana na wenzake katika kutengeneza mashambulizi.

Mchezo dhidi ya TRA United ulimpa nafasi nyingine ya kuonyesha ubora wake akicheza kwa kujiamini na kushiriki katika ujenzi wa mashambulizi ya timu yake na aliendelea kuonyesha kiwango kizuri pia katika mchezo dhidi ya Namungo ambapo alidhihirisha ukomavu mkubwa licha ya kuwa bado ni mmoja wa wachezaji wenye umri mdogo kikosini.

Kilichowavutia wengi si tu uwezo wake wa kucheza bali namna anavyobeba majukumu bila kuonekana kutishwa na ukubwa wa mechi, anaonekana kuwa mchezaji anayependa mpira ukiwa miguuni mwake, mwenye ujasiri wa kufanya maamuzi na anayejifunza kwa haraka kila anapopewa nafasi huku akiwa ndiye mchezaji mdogo zaidi mwenye mabao mengi msimu huu akifunga mawili.

Safari yake imeanzia Fountain Gate Sports Academy, mfumo ambao umeendelea kuzalisha vipaji vya kiwango cha juu nchini na kupandishwa kwake hadi kikosi cha wakubwa ni matokeo ya kazi, nidhamu na maendeleo aliyoyaonyesha tangu akiwa kwenye timu za vijana na pia amewahi kuwa sehemu ya timu za vijana za Tanzania, jambo linalodhihirisha kuwa uwezo wake umetambuliwa mapema.

Kwa kasi ya maendeleo yake wengi wanaamini Juma Issa Abushiri ana kila sababu ya kuwa mmoja wa nyota watakaobeba bendera ya soka la Tanzania katika miaka ijayo, akiendelea kupata muda wa kucheza, kufanya kazi kwa bidii na kujifunza kutoka kwa wachezaji wenye uzoefu, hakuna shaka kuwa safari yake inaelekea kwenye hatua kubwa zaidi.

Mwezi Juni umekuwa kipindi kingine muhimu katika ukuaji wake, ingawa bado ana safari ndefu mbele yake, kiwango alichokionyesha kinathibitisha kuwa Tanzania inaendelea kupata kizazi kipya cha wachezaji wenye uwezo wa kufanya makubwa ndani na nje ya nchi.





Vinara wa takwimu Ligi Kuu ya NBC 2025/2026

Kinara wa Mabao

NDUMUMWE MOSSI

Michezo	12
Dakika	1802
Mabao	17



Kinara wa Hati safi



DJIGUI DIARA

Michezo	24
Dakika	2160
Hati Safi	18

Kinara wa Pasi Saidizi

ELIE MPANZU

Michezo	25
Dakika	1448
Pasi za Mabao	10



Kinara wa Kuhusika kwenye Mabao



FEISAL SALUM

Michezo	28
Dakika	2202
Mabao	15
Pasi za Mabao	9
Mabao Aliyohusika	24



Iddi Seleman

‘BOLI’ & ‘FASHENI’



Ettiene Ndairagije



NBC CHAMPIONSHIP LEAGUE

championshiptz



SAFARI YA GEITA GOLD HADI LIGI KUU YA NBC.

Haikuwa safari nyepesi kwa Geita Gold kupanda Ligi Kuu ya NBC msimu huu kutokana na ushindani ulivyokuwa katika Ligi ya NBC Championship ikiwa imeizidi timu ya Kagera Sugar alama tano huku Polisi Tanzania na Mbeya Kwanza zikisubiri kucheza hatua ya mtoano na timu za Ligi Kuu ambazo zitamaliza kwenye nafasi za mtoano katika msimamo.

Baada ya kushuka Daraja msimu wa 2023/24 ikiwa na alama 25 ambapo katika mechi 30, ilishinda tano, sare 10, na kufungwa 15, msimu uliyofuata wa 2024/25 ilicheza NBC Championship lakini haikufanikiwa kupanda ikimaliza nafasi ya nne na alama 56 zilizowafanya kupata nafasi ya kucheza michezo ya mtoano na haikuweza kupanda daraja badala yake zilipanda timu za Mtibwa Sugar na Mbeya City.

'Wachimba dhahabu' hao walijipanga zaidi msimu huu wakiwa vinara kwa alama 77 katika michezo 30, wakishinda 24, sare tano na kufungwa mmoja huku wakifunga mabao 68 na mabao ya kufungwa 17 na majirani zao wa Kagera Sugar wakimaliza nafasi ya pili kwa alama 72.

Sio mara ya kwanza kwa Geita kushuka na kupanda Daraja ikifanya hivyo msimu wa 2020/21 na rekodi nyingine ni kwa kocha mkuu wa timu hiyo Zuberi Katwila ambaye mbali na kuipandisha Geita timu nyingine aliyowahi kuipandisha ni Ihefu ambayo kwa sasa inajulikana kama Singida Black Stars.

Timu hiyo pia imetoa mshambuliaji kinara akiwa na mabao 18 Maulid Shabani akifuatiwa na nyota raia wa Zambia anayecheza Kagera Sugar Obrey Chirwa aliyemaliza na mabao 17.

Ukiachana na hilo, moja ya silaha iliyotumia Geita kupanda katika michezo 15 iliyocheza kwenye uwanja wake wa Nyankumbu haikupoteza mchezo wowote, ilishinda 12 na sare tatu hivyo kukusanya jumla ya alama 39 wakati mechi za ugenini timu hiyo ilishinda 12, sare mbili na kufungwa mmoja katika michezo 15, hivyo kufanikiwa kukusanya alama 38 za ugenini.

Kocha Zuberi Katwila anasimulia safari ya kusaka nafasi ya kupanda Ligi Kuu akisema haikuwa rahisi, lakini utayari wa wachezaji kupokea mbinu na kuzifanyia kazi kwa kujituma wamefanikiwa kutimiza malengo ya timu.

"Ligi ya NBC Championship siyo rahisi, lakini kwa umoja wa wachezaji, viongozi na benchi la ufundi tumefanikisha kwa pamoja kufikia malengo japo changamoto ya ushindani ilikuwepo kwa kiasi kikubwa sana."alisema Katwila.

Mshambuliaji na nahodha wa timu hiyo, Yussufu Mhilu aliyemaliza na mabao matano anasema:"Ligi ya NBC Championship siyo rahisi, lakini furaha yetu ni kuona timu imepanda Ligi Kuu ya NBC na mashabiki wa Geita wamepata furaha waliyoikosa kwa kipindi kirefu."



Namba zao zimetikisa NBC Championship 2025/2026

Simulizi nyingi za ushindani, mafanikio na vipaji kutoka kona mbalimbali za Tanzania imeachwa na Ligi ya Championship ya NBC msimu wa 2025/26 iliyomalizika Juni 19.

Licha ya vita ya kupanda Ligi Kuu ya NBC kulikuwa na nyota waliweka rekodi zao zilizowafanya kuwa vinara katika nafasi zao. Kuanzia kwa kinara wa ‘kucheka na nyavu’, golikipa na mwamba aliyecheza dakika nyingi zaidi msimu wa 2025/26.

Mbio za ufungaji zilikuwa za kibabe hadi dakika za mwisho ambapo Obrey Chirwa wa timu ya Kagera Sugar na Maulid Shabani wa Geita Gold walimaliza msimu wakiwa wamefunga mabao 18 kila mmoja, wakigawana heshima ya kuwa wafungaji bora wa NBC Championship 2025/26.

Chirwa aliyewahi kuzitumikia timu za Young Africans, Azam na Ken Gold kwa nyakati tofauti kwenye Ligi Kuu ya NBC, katika michezo 24 na dakika 1,584 alizocheza aliweza kufunga mabao 18, wastani unaoonyesha kuwa alikuwa mchezaji wa kulindwa kila alipokanyaga uwanjani na uwezo wake wa kutumia nafasi chache na kuzigeuza kuwa mabao ulimfanya kuwa mmoja wa washambuliaji hatari zaidi msimu huu.
Kwa upande mwingine, Maulid Shabani alicheza michezo 30 ikiwa ni jumla ya dakika 2,355 na kufunga mabao 18 sawa na Chirwa huku mchango wake ukiwa mkubwa kwa ‘wachimba dhahabu’ kutwaa ubingwa msimu huu.



Obrey Chirwa



Maulid Shaban

Katika upande wa magolikipa jina la Paul Kamtewe wa timu ya Mbuni kutoka mkoani Arusha liliibuka kinara juu ya wote ambapo katika michezo 24 aliyocheza kwa dakika 2,067, aliweka rekodi ya kufikisha hati safi 12 ikimaanisha nusu ya mechi alizocheza hakuruhusu bao.
Kamtewe alikuwa msingi mkubwa wa mafanikio ya Mbuni iliyomaliza nafasi ya sita kwenye msimamo kutokana na utulivu wake, uwezo wa kusoma mchezo na kufanya maamuzi sahihi katika nyakati muhimu huku rekodi yake ikionyesha kuwa mafanikio ya timu hayajengwi na wachezaji wa ndani pekee bali hata golikipa ni nguzo muhimu kwenye timu.
Katika soka la kisasa, uimara wa mchezaji hupimwa pia kwa uwezo wake wa kudumu uwanjani na kustahimili ‘mshikemshike’ wa dakika 90 bila kuchoka na hilo ndilo lililomtofautisha Geofrey Joel Koroso wa Kengold aliyecheza dakika nyingi kuliko mchezaji yeyote kwenye Ligi ya Championship ya NBC.
Mchezaji huyo alicheza michezo 30 ikiwa jumla ya dakika 2,645, idadi kubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote katika NBC Championship msimu huu, rekodi hiyo inaonyesha kiwango kikubwa cha utimamu wa mwili aliyokuwa nayo ‘mwamba’ huyo.



Paul Kamtewe



Geofrey Koroso

Wababe wa ‘Kanda ya Ziwa’ warejea Ligi Kuu ya NBC

Msimu wa Ligi ya Championship ya NBC 2025/26 umefikia tamati ukiwa umejaa ushindani baina ya timu, msisimko na mapambano makali ya kutafuta nafasi ya kucheza Ligi Kuu ya NBC.

Baada ya safari ya miezi kadhaa na michezo 30 kwa kila klabu, timu za Geita Gold na Kagera Sugar zimefanikiwa kupata tiketi ya kupanda daraja.

Geita Gold wamehitimisha msimu kwa kutwaa ubingwa wa NBC Championship baada ya kukusanya alama 77, wakithibitisha kuwa walikuwa timu bora zaidi katika msimu wa 2025/26.

Katika mechi zao 30 walishinda 24, sare tano na kupoteza mchezo mmoja pekee kiwango kilichowawezesha kujenga pengo la alama dhidi ya wapinzani wao na kuhakikisha wanamaliza kileleni mwa msimamo wa ligi.

Mbali na matokeo hayo Geita Gold walionyesha ubora mkubwa katika pande zote mbili za mchezo, walifunga mabao 68, idadi iliyowafanya kuwa timu iliyofunga mabao mengi huku wakiruhusu mabao 17 pekee na kuwa timu ya pili kufungwa mabao machache nyuma ya Kagera Sugar iliyofungwa 12.

Kupanda kwa Geita Gold kunamaanisha kurejea kwa klabu hiyo yenye maskani yake Nyankumbu, Geita katika Ligi Kuu ya NBC ikiwa na matarajio ya kufanya vizuri na kurejesha ushindani dhidi ya ‘vigogo’ wa soka la Tanzania.

Upande mwingine timu ya Kagera Sugar imeandika simulizi yao ya mafanikio kwa kurejea Ligi Kuu ya NBC baada ya kumaliza katika nafasi ya pili ikukusanya alama 72 ambapo katika michezo yao 30, walishinda 24, wakatoka sare sita, huku wakimaliza msimu bila kupoteza hata mchezo mmoja na kuweka rekodi ya kutofungwa katika msimu mzima ikiwa ni ishara ya kiwango cha juu cha ubora, nidhamu ya kiuchezaji na uwezo mkubwa wa kupata matokeo katika kila hatua ya ligi.

Kagera ilikuwa timu ya pili kwa kufunga mabao nyuma ya Geita ikiwa nayo 53, huku ikiwa timu iliyofungwa mabao machache 12 pekee.

Upande wa chini ya msimamo wa Ligi ya Championship ya NBC safari ya timu za Barberian na Hausung katika Ligi hiyo imefikia tamati baada ya timu hizo kushindwa kujinusuru na ‘mkasi’ wa kushuka daraja na kumaliza katika nafasi mbili za mwisho kwenye msimamo na hivyo kushiriki First League msimu wa 2026/27.

Barberian walimaliza katika nafasi ya 15 wakiwa na alama 18, wakishinda mechi tatu, sare tisa na kupoteza michezo 18 huku katika kipindi chote cha msimu walifunga mabao 18 pekee na kuruhusu mabao 43.

Kwa upande wa Hausung walimaliza mkiani mwa msimamo katika nafasi ya 16 wakiwa na alama tisa baada ya kushinda mechi tatu, kutoka sare tatu na kupoteza 24 huku ikifunga mabao 16 na kuwa timu iliyofunga mabao machache na pia ikifungwa mabao 62 na kuwa safu ya ulinzi iliyoruhusu mabao mengi zaidi msimu huu.

Kushuka kwa Barberian na Hausung kunafunga ukurasa wa msimu uliokuwa na changamoto nyingi kwa timu hizo huku zikilazimika kujipanga upya kwa ajili ya First League na wakati timu hizo zikianza maandalizi ya safari mpya, nafasi zao katika NBC Championship





First League

firstleaguetz



Rhino Bingwa First League 2025/26.

Msimu wa First League 2025/26 umefikia tamati kwa ushindani ulioshuhudia klabu mbili zikitimiza ndoto ya kupanda daraja na nyingine mbili zikiaga mashindano hayo huku wababe kutoka Tabora timu ya Rhino Rangers ikiibuka mabingwa.

Rhino Rangers na Bandari wamefanikiwa kupanda NBC Championship msimu wa 2026/27.

Msimu huu umedhihirisha ushindani unaozidi kuongezeka katika First League, ligi ambayo imeendelea kuwa daraja muhimu la kuzalisha wachezaji wenye uwezo wa kushindana katika ngazi za juu za soka la Tanzania.

Rhino Rangers iliyomaliza kinara wa Kundi B kwa kukusanya alama 35 baada ya kucheza michezo 14, ikishinda michezo 11, kutoka sare mbili na kupoteza mmoja pekee.

Katika kipindi hicho walifunga mabao 31, huku wakiruhusu mabao tisa ikiwa ni takwimu zilizodhihirisha ubora wao katika ushambuliaji na uimara wa safu ya ulinzi na kuwawezesha kuvuka hatua za mtoano hadi kufika fainali wakiwa miongoni mwa timu zilizokuwa na kiwango bora zaidi msimu huu.

Katika mchezo wa fainali Rhino Rangers walikabiliana na Bandari katika pambano lililotoa burudani kubwa kwa mashabiki baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 na mshindi kupatikana kupitia mikwaju ya penalti ambapo Rhino Rangers walionyesha

utulivu mkubwa na kushinda kwa mikwaju ya penati 4-2 hivyo kutwaa ubingwa wa First League 2025/26.

Ubingwa huo unaweka alama ya mafanikio kwa Rhino Rangers na kuwapa nafasi ya kuingia NBC Championship wakiwa na morali kubwa pamoja na matarajio ya kuendelea kufanya vizuri katika ngazi ya juu zaidi ya ushindani.

Wakati huo timu ya Bandari ilikuwa na msimu wa mafanikio baada ya kumaliza vinara wa Kundi A kwa alama 32 wakishinda michezo 10, kutoka sare miwili na kupoteza miwili huku wakifunga mabao 25 na kuruhusu tisa.
Baada ya kufuzu hatua za mtoano Bandari waliendelea kuonyesha kiwango kizuri hadi kufika fainali ingawa walishindwa kutwaa ubingwa baada ya kupoteza dhidi ya Rhino.
Kupanda kwa Bandari kunarejesha matumaini mapya kwa klabu hiyo kuelekea msimu wa 2026/27 ambapo itakuwa na nafasi ya kupambana katika ushindani wa NBC Championship ikiwa na lengo la kuendelea kupiga hatua hadi kupanda Ligi Kuu ya NBC kwa misimu inayofuata.

Mchezo wa fainali ulikuwa kilele cha msimu wa First League 2025/26 kati ya Rhino Rangers na Bandari walioonyesha ubora wa kiufundi, nidhamu na ari ya ushindani katika mchezo uliokuwa na kasi na ushambuliaji wa kuvutia na ilikuwa timu ya Rhino iliyofanikiwa kuondoka na Ubingwa wa First League.
Sare ya mabao 2-2 ndani ya muda wa kawaida ilionyesha jinsi timu hizo zilivyokuwa na viwango vinavyokaribiana na hata hivyo mikwaju ya penalti ndiyo iliyoamua hatima ya ubingwa huku Rhino Rangers wakitumia vizuri penati zao na kuibuka mabingwa kwa ushindi wa 4-2.
Fainali hiyo ilitoa taswira ya ubora wa timu zilizopanda daraja na kuonyesha kiwango cha ushindani kinachoendelea kuimarika katika First League.





‘Wakali’ wa ‘kufumania’ nyavu First League 2025/2026.

First League msimu wa 2025/26 umeacha kumbukumbu ya ushindani mkubwa na kuibua washambuliaji waliogeuka nguzo muhimu za timu zao. Kila bao walilofunga halikuwa tu takwimu kwenye karatasi, bali lilibeba matumaini ya ushindi, alama tatu na ndoto za kupanda daraja kuelekea Ligi ya Championship ya NBC.

George William Komba wa Rhino Rangers ndiye aliyeng'ara zaidi kwenye suala la kufunga mabao baada ya kufunga 11 katika michezo 14 aliyocheza, akitumia dakika 1,256 pekee.

Mshambuliaji huyo alikuwa silaha kuu ya Rhino akionyesha utulivu mkubwa ndani ya eneo la hatari na uwezo wa kutumia nafasi anazopata huku mabao yake yakiwa sehemu muhimu ya safari ya mafanikio ya timu hiyo iliyomaliza msimu ikiwa bingwa na kupanda kushiriki NBC Championship msimu ujao.

Nyuma yake walifuatia Danford Mosses Kaswa wa Bandari na Ally Hamisi Mwinjuma wa NKIM, ambao kila mmoja alimaliza msimu akiwa na mabao 8. Kaswa alifikia idadi hiyo ndani ya michezo 12 yenye dakika 769 jambo linaloonyesha kiwango cha juu cha ufanisi kila alipopata nafasi ya kucheza huku kwa upande wa Mwinjuma mabao yake nane alifunga kwenye michezo 11 iliyokuwa na jumla ya dakika 969.

Mohamed Rajab Vuai wa Cosmopolitan na Pasco Miligo Yasata wa IAA walifunga mabao 7 kila mmoja, ambapo Vuai alifunga idadi hiyo katika michezo 13, huku Yasata akifanya hivyo ndani ya michezo 12.

Mbali na idadi ya mabao yao waliyofunga, washambuliaji hawa waliipa First League mvuto mkubwa kwa ushindani wao wa kila wiki. Walizifanya safu za ulinzi za wapinzani kuwa kwenye tahadhari muda wote hawa ‘wataalamu’ wanapokuwa uwanjani na kuwapa mashabiki burudani kupitia uwezo wao wa kumalizia mashambulizi, uwepo wao uliifanya vita ya ufungaji kuwa moja ya vivutio vikubwa.

Kwa baadhi ya washambuliaji waliofanya vizuri huu unaweza kuwa mwanzo wa safari kuelekea ngazi ya juu zaidi za soka la Tanzania, huku kwa wengine ukiwa msingi wa kujenga mafanikio makubwa zaidi katika misimu ijayo. Wote kwa pamoja wameonyesha kwamba First League inaendelea kuwa jukwaa muhimu la kuibua vipaji na kuzalisha washambuliaji wenye uwezo wa kung'ara katika soka la Tanzania.



Zijue Kanuni



Kanuni: 9 (2)

Katika kutambulisha uwanja wake wa nyumbani, klabu inawajibika kuhakikisha kuwa uwanja huo unakidhi vigezo vyote na masharti kama vilivyoainishwa kwenye kanuni za leseni za klabu.

Tuzo za Mwezi msimu 2025/2026

Mwezi	Mchezaji Bora	Klabu	Kocha Bora	Klabu
Septemba 2025	Djigui Diarra	Young Africans	Ahmad Ali	JKT Tanzania
Oktoba 2025	Issa Abushiri	Fountain Gate	Mohammed Laizer	Fountain Gate
Novemba 2025	Fabrice Ngoy	Namungo	Juma Mgunda	Namungo
Desemba 2025	Duke Abuya	Young Africans	Pedro Gonçalves	Young Africans
Januari 2026	William Edger	Dodoma Jiji	Pedro Gonçalves	Young Africans
Februari 2026	Laurindo Dilson	Yanga	Steve Barker	Simba
Machi 2026	Ibrahim Imoro	Singida Black Stars	Steve Barker	Simba
Aprili 2026	Allan Okello	Young Africans	Pedro Gonçalves	Young Africans
Mei 2026	Allan Okello	Young Africans	Steve Barker	Simba
Juni 2026	Mossi Ndumumwe	Singida BS	Abdihamid Moallin	Young Africans

Msimu 2026/2027

	MASHINDANO YA KIMATAFA
	CAF CONFEDERATION
1	AZAM FC
2	SINGIDA BLACK STARS
	CAF CHAMPIONS LEAGUE
1	YOUNG AFRICANS
2	SIMBA SC

	LIGI KUU YA NBC	
	TIMU ZILIZOPANDA DARAJA	**TIMU ZILIZOSHUKA DARAJA**
1	GEITA GOLD	KMC
2	KAGERA SUGAR	MTIBWA SUGAR
3	POLISI TANZANIA	TANZANIA PRISONS

	LIGI YA CHAMPIONSHIP YA NBC	
	TIMU ZILIZOPANDA DARAJA	**TIMU ZILIZOSHUKA DARAJA**
1	RHINO RANGERS	HAUSUNG
2	BANDARI FC	BARBERIAN
3	IAA SC	AFRICAN SPORTS

	FIRST LEAGUE	
	TIMU ZILIZOPANDA DARAJA	**TIMU ZILIZOSHUKA DARAJA**
1	KAJUNA FC	GREEN WARRIORS
2	KAHAMA MADINI	BIASHARA UNITED
3	MT. HANANG	MAPINDUZI



Ahsanteni Wadhamini na Wadau Wetu

Msimu wa Ligi Kuu ya NBC 2025/2026 umehitimishwa kwa mafanikio makubwa yaliyowezekana kutokana na ushirikiano, kujitolea na imani ya wadau mbalimbali walioendelea kusimama nasi katika safari hii.

Bodi ya Ligi Kuu Tanzania inatoa shukrani za dhati kwa benki ya Taifa ya biashara (NBC) kwa kuendelea kuwa Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya NBC na mshirika muhimu katika kukuza na kuendeleza soka la Tanzania.

Tunawashukuru Azam Media Limited, Mdhamini mwenye haki ya Matangazo ya Televisheni, kwa kuwafikishia mamilioni ya mashabiki burudani ya Ligi Kuu ya NBC kupitia matangazo ya kiwango cha juu.

Tunatoa shukrani kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Mdhamini mwenye haki ya Matangazo ya Redio, kwa kuendelea kuisogeza ligi karibu na Watanzania kupitia matangazo ya moja kwa moja, taarifa na vipindi mbalimbali vya michezo.

Shukrani za pekee pia ziende kwa Just Fit Sports Gear, Mdhamini wa Sare za Waamuzi na Mpira Rasmi wa Ligi, kwa mchango wake katika kuhakikisha mashindano yanaendeshwa kwa viwango vya juu na kwa kutumia vifaa vinavyokidhi hadhi ya Ligi Kuu ya NBC.

Aidha, tunalishukuru Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), klabu zote zilizoshiriki, waamuzi, makamishna wa mechi, vyombo vya habari, vyombo vya ulinzi na usalama, watoa huduma, pamoja na mamilioni ya mashabiki wa soka nchini kwa ushirikiano wao mkubwa ulioifanya ligi kuwa ya ushindani, yenye ubora na mafanikio.

Asanteni kwa kuwa sehemu ya mafanikio ya Ligi Kuu ya NBC 2025/2026. Ushirikiano wenu ndiyo nguvu ya maendeleo ya soka letu. Tunatazamia kuendelea kujenga pamoja ligi yenye hadhi, ushindani na mafanikio makubwa zaidi katika misimu ijayo

NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

azamtv

JUSTFIT Sports Gear

TBC
Ukweli na Uhakika

TUNAKUONA MBALI

NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

Familiaaa, Burudani za Soka Zisikupite

Lipia king'amuzi chap kupitia **NBC Kiganjani**



Pakua App ya NBC Kiganjani au Piga *150*55# > Tv.